TANGAZO LA SERIKALI NA. 124 la tarehe 24/2/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI

(SURA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa Chini ya Kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA KINYAMSHINDO YA MWAKA, 2023.

Jina:

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Kinyamshindo ya mwaka, 2023

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura (355)

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mipango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba.

**JEDWALI**

(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)
Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo:-

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KM1 yenye majira – nukta 741271.691MS, 9441549.184KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KZ54$^{0}$03'45.67''MS kwa umbali wa kilomita 1.22 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KM2 yenye

*Tangazo la Serikali na.124 (linaendelea)*

majira – nukta 742265.710MS, 9440828.648KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini katika uelekeo wa KS5$^0$47’25.73’’ kwa umbali wa kilomita 5.74 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba KM3 yenye majira - nukta 741686.571MS, 9435117.700KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi kwa kukatiza barabara ya Kinyamshindo-Mengu katika uelekeo wa S49$^0$40’02.98’’W kwa umbali wa kilomita 3.28 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KM4 yenye majira – nukta 739179.512MS, 9432989.112KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS7$^0$83’15.63’’MG kwa umbali wa kilomita 2.00 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KM5 yenye majira – nukta 737167.684MS, 9432747.590KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS83$^0$12’43.04’’MG kwa umbali wa kilomita 2.4 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KM6 yenye majira – nukta 734743.684MS, 9432459.082MG; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki kwa kukatiza barabara ya Singida – Kinyamshindo katika uelekeo wa KZ35$^0$41’01.72’’MS kwa umbali wa kilomita 11.19 hadi ulipoanzia.

Dodoma,
6 February, 2023

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*